

OFISI YA RAIS-TAMISEMI

HALMASHURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KAJUNJUMELE

S.L.P531

KYELA

03/12/2021

Kumb. NA.KML/FI/VOL2/2021

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

KYELA

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAJUNJUMELE MWAKA 2021**

1.0. UTANGULIZI

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka 2020. Shule ya sekondari Kajunjumele ipo umbali wa **km3** mashariki mwa mji wa Kyela. mhula wa kwanza wa masomo utanza tarehe **11/01/2021**, unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 6/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2020. unatakiwa kufika bila kukosa.

2.0. MAMBO MUHIMU YAKUZINGATIA

2.1. SARE ZASHULE

(A) WAVULANA.

Suruali mbili, moja ya rangi ya **kijivu** na nyingine rangi ya **dark blue** (ona kitambaa), mashati mawili meupe mikono mifupi.

(B) WASICHANA.

sketi mbili (ndefu), moja ya rangi ya **kijivu** na nyingine ya rangi ya **dark blue** (ona kitambaa), mashati mawili **meupe** mikono mifupi.

-Hijabu (waislamu) kitambaa lazima kifanane na rangi ya shati.

WOTE

(A) Viatu vya ngozi nyeusi, vifungwavyo kwa kamba: jozi mbili. Ni marufuku kuvaa viatu vya plastiki (yeboyebo).

(b) Soksi nyeupe ndefu (wasichana) na nyeusi (wawulana).

(c) Sare za michezo ni tract suit ya blue bahari na viatu vyamichezo.

(d) Tisheti dark blue ya kola yenye ufito wa kijivu kwenye kola na mikono.

2.2. Daftari za kutosha (**counter book**), kalamu na mkebe wahisabati.

2.3. Chakula cha wanafunzi (wa kutwa), nauli ya kwenda shuleni na kurudinyumbani pamoja na matibabu.

2.4. Mzazi au mlezi anapaswa kuhudhuria vikao vyote vya wazazi vinanyoitishwauleni.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULEHII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi Teknolojia na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora yenye majukumu ya usimamizi na uendeshaji elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na mazingira kikamilifu maelekezo juu ya kuweponan.
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira yashule
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba yashule
- i) Kutunza mali za umma

3.1 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- A. Wizi.
- B. Uasherati.
- C. Ubakaji.
- D. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- E. Kupigana aukupiga.
- F. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- G. Kudharau bendera ya taifa.
- H. Kuwamjamzito.
- I. Kuo aukuolewa.
- J. Kutoa mimba.
- K. Kugoma kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- L. Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 MAMBO MENGINE YA MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NAMWANAFUNZI.

(A) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipotishuleni

(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa yajinai

(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na maelekezo mengine yatakayotolewa nashule

5.0. TAFADHARISOMAKWAMAKINIMAELEZO/MAAGIZOHAYANAKUYATEKELEZAKIKAMILIFU

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

G. S. NDANAA

MKUU WA SHULE

0755202068/0715436186